TANGAZO LA SERIKALI Na. 792 La Tarehe. 6/9/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI YA MWAKA 2024

Jina

1.Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yatakayolipwa na mtu yeyote kwa Halmashauri kwa ajili ya kupata kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Pangani;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"maeneo yasiyoruhusiwa" maana yake ni maeneo ya mito, madaraja, barabara, mashamba ya watu, mijini pamoja na maeneo mengine yanayofanana na hayo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani na ni pamoja na afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu kwa niaba ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli zinazohusu ununuzi wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni au asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru wa madini ya ujenzi kwa niaba yake.

Wajibu wa Halmashauri

4.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kupokea taarifa za maeneo yote yanayokusudiwa kuanzishwa machimbo ya madini ya ujenzi na kuyakagua ili kujiridhisha kama maeneo yaliyotolewa taarifa yametengwa kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Kusimamia shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi ili kuhakikisha kuwa uchimbaji unafanyika kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa ili kuzuia uharibifu wa mazingira.

Maombi ya kibali cha uchimbaji

5.-(1) Mtu, taasisi au kampuni inayokusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri itatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi maombi ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kupitia fomu maalum itakayotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Maombi ya kibali yatakayowasilishwa kwa Halmashauri yatatakiwa kuambatishwa na taarifa zifuatazo:

(a) leseni ya uchimbaji wa madini iliyotolewa na mamlaka husika;
(b) aina ya madini yanayokusudiwa kuchimbwa;
(c) umiliki pamoja na ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi;
(d) mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la machimbo; na
(e) muhtasari wa kijiji ambacho uchimbaji wa madini ya ujenzi utafanyika ukionyesha kukubaliana na uchimbaji huo.

(3) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hii kitaeleza aina ya madini yanayochimbwa na eneo litakalochimbwa madini hayo na kitalipiwa ada kwa kiwango

kilichoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

Uwezo wa kufunga machimbo

6.-(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga machimbo yoyote ya madini ya ujenzi kama itaona kufanya hivyo ni kwa maslahi ya Halmashauri na umma kwa ujumla.

(2) Kabla ya kufunga machimbo yoyote, Halmashauri itatoa notisi kwa madhumuni ya kuwataarifu wakazi wa Halmashauri kuhusu kusudio hilo.

Ushuru wa madini ya ujenzi

7-(1) Mtu yeyote atakayesafirisha madini ya ujenzi kutoka eneo yalikochimbwa kwenda maeneo mengine atalipa ushuru kwa tani kulingana na viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(2) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa mara baada ya msafirishaji kununua madini kutoka kwa mchimbaji au kupakia madini hayo katika chombo ambacho atakitumia kwa ajili ya kusafirishia.

(3) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo, barabara zinazoelekea au kutoka maeneo ya machimbo au eneo lolote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.

(4) Mnunuzi yeyote atakayeshindwa kulipa ushuru anaotakiwa kulipa atatakiwa kupakua madini ya ujenzi kutoka katika chombo au kutochukua madini hayo mpaka hapo atakapolipa ushuru anaodaiwa.

Wajibu wa kulipa

8.-(1) Kila mtu anayestahili kulipa

ushuru

ushuru atakuwa na wajibu wa kulipa ushuru huo kama ilivyoelekezwa katika Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumzuia dereva wa gari lolote kujishughulisha na usafirishaji wa madini ya ujenzi ikithibitika kwamba kuna ukiukwaji na uvunjaji wa Sheria Ndogo hii.

(3) Ushuru wa madini ya ujenzi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo hayo.

(4) Kila mtu aliyelipa ushuru atakuwa na wajibu wa kudai stakabadhi na haitakuwa utetezi kwa mtu yeyote kudai kuwa amelipa ushuru lakini hakupewa stakabadhi.

Muda wa machimbo kuwa wazi na kusafirisha madini ya ujenzi

9.-(1) Shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri zitafanyika kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni ya kila siku.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalum kuruhusu shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi kufanyika nje ya muda ulioainishwa.

(3) Kila mmiliki wa gari linalosafirisha madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha kuwa wakati wote wa usafirishaji wa madini ya ujenzi gari hilo limefunikwa ili kuzuia uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Vituo vya ukaguzi

10.-(1) Halmashauri itaanzisha vituo kwa

ajili ya ukaguzi wa magari yanayobeba madini ya ujenzi katika njia zinazoingia na kutoka katika maeneo ya machimbo.

(2) Kila dereva wa gari linalosafirisha madini ya ujenzi atakuwa na wajibu wa kusimama katika kituo cha ukaguzi wa madini ya ujenzi na kuonesha stakabadhi ya kielektroniki aliyolipia ushuru na endapo hatakuwa na stakabadhi hiyo atatakiwa kulipa ushuru kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Halmashauri kutowajibika kwa hasara

11. Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote atakayopata mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi wakati wa kukusanya ushuru isipokuwa kama hasara hiyo itatokana na uzembe wa afisa yeyote wa Halmashauri.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

12. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote linalochimbwa madini ya ujenzi muda wa saa za kazi kwa ajili ya kukagua na kukusanya ushuru.

Wakala

13. Halmashauri inaweza kuteua wakala ili kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Kufutwa au kusimamishwa kwa kibali

14.-(1) Halmashauri inaweza kufuta au kusimamisha kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi endapo itajiridhisha kuwa kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii au masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya

ujenzi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), kabla ya kufuta au kusimamisha kibali Halmashauri itatakiwa kutoa notisi ya siku saba kwa mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali cha kusudio la kufuta au kusimamisha kibali.

(3) Notisi itakayotolewa chini ya kanuni hii itaainisha sababu za kufuta au kusimamisha kibali husika.

(4) Endapo kibali kitafutwa au kusimamishwa, mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi itakoma kuchimba madini hayo.

Makosa na adhabu

15. Mtu yeyote ambaye-

(a) anakataa au kushindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Mwidhiniwa;

(b) anamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(c) anakataa au anakwepa kulipa ushuru;

(d) anashawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru;

(e) anachimba madini ya ujenzi katika maeneo yasiyoidhinishwa au yasiyoruhusiwa na Halmashauri;

(f) anaanzisha machimbo ya madini ya ujenzi bila kuwa na kibali kutoka Halmashauri;

(g) anapeleka maombi ya leseni ya madini ya ujenzi Wizara ya Madini bila kujadiliwa na kuridhiwa na kijiji

husika na kupitishwa na Halmashauri;

(h) anasafirisha madini ya ujenzi bila kulipa ushuru;

(i) anachimba madini ya ujenzi kabla au baada ya muda ulioruhusiwa kuchimba; au

(j) anasafirisha madini ya ujenzi katika gari ambalo halijafunikwa,

anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

16. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume na Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(1))*

KIBALI CHA KUCHIMBA MADINI YA UJENZI

NDUGU; …………………………………..…
S.L.P………………………………………….
…………………………………....

Yah: KIBALI CHA KUCHIMBA MADINI YA UJENZI

Kibali kinatolewa kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo kama ulivyoomba kwa mujibu wa Sheria. Kibali hiki ni kwa ajili ya kuchimba ……………..………………………………………………………………………. (mawe, mchanga, kokoto, kifusi, udongo, madini mengine). Katika eneo la shamba/kiwanja lililopo/kilichopo Kitongoji cha …………………………. Kijiji cha ……………………………….Kata ya…………….………………... Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. Kibali hiki kitatumika kuanzia tarehe ………………….. hadi tarehe ………………………………. na kwamba kibali hiki kitatumika katika eneo lililoainishwa tu katika kibali hiki. Kibali hiki kinatolewa kwa wamiliki au watu/kampuni walioingia mkataba na mmiliki/wamiliki wa eneo linaloombewa kibali.

MAONI YA AFISA MAZINGIRA
Kibali kitolewe/kisitolewe, kwani tathmini ya mazingira imefanyika/haijafanyika na imebaini kutakuwa/hakutakuwa na uharibifu wa Mazingira.
Jina: …………………………………………………..
Cheo: ……………………………………………………
Saini: ……………………………………………………
Tarehe: …………………………………………………

MAONI YA AFISA MIPANGO MIJI
Kibali kitolewe/kisitolewe, kwani uchimbaji kwenye eneo hilo mpango wa matumizi yake utaathiri/hautaathiri upangaji miji.
Jina: …………………………………………………..
Cheo: ……………………………………………………
Saini: ……………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 792 (Linaendelea.)*

Tarehe: …………………………………………………

(N.B) kibali kijazwe nakala mbili moja apatiwe msafirishaji na nyingine iwasilishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W).

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(3))*

ADA YA KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

| NA | ADA | KIWANGO (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kibali cha kumiliki eneo la kuchimba madini ya ujenzi | 1,000,000/= kwa kila kibali |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1))*

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| NA | AINA YA MADINI | KIWANGO (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Tarazo | 5,000/= kwa tani |
| 2. | Mawe | 5,000/= kwa tani |
| 3. | Moramu | 4,000/= kwa tani |
| 4. | Kokoto | 6,000/= kwa tani |
| 5. | Udongo au kifusi | 4,000/= kwa tani |
| 7. | Mchanga | 6,000/= kwa tani |
| 8. | Madini mengine | 6,000/= kwa tani |

JEDWALI LA NNE

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16*)

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……..…. mwaka ……..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi …………….. kama ushuru ninaodaiwa na kiasi cha shilingi …………………. kama faini ya ufifilishaji wa kosa badala ya kupelekwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.
Leo tarehe………….ya Mwezi…………..… Mwaka ……………..………….

Jina……………………………….. Saini…………………………………….

MBELE YANGU :
Jina: …………………………………..……………………
Saini………………………..…………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ulibandikwa kwenye sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 29/4/2022 mbele ya:-

ISAYA MUGISHANGWE MBENJE,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*PANGANI*

AKIDA OMARI BAHORARE,
*Mwenyekiti,*
*Halmahsuair ya wilaya,*
*PANGANI*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
30 Novemba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.),
Waziri wa Nchi-OR-Tamisemi,